**MUHULA WA PILI 2023**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI(102/2)**
**KIDATO CHA NNE (4)**
**MUDA: SAA 2 ½**

**Maagizo**

1. Jibu maswali yote.
2. Majibu yote yaandikwe kwenye sehemu ulizoachiwa.
3. Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

Kwa matumizi yam tahini pekee

| SEHEMU | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

**1.UFAHAMU(ALAMA 15)**
***Soma kifungu kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Teacher.co.ke

Hapo zamani palikuwa na nchi iitwayo Matunda.Nchi hii ilikabiliwa na umaskini mkubwa. Hata katika mashaka hayo, viongozi wa Matunda hawakusahau kuwa akili ni mali.Wazee waliitwa ili kutumia hekima yao ili kufumbua tatizo la umaskini .Kila mzee alijikuna kichwa mpaka akaambua nywele lakini wapi.
Uliitishwa mkutano mkubwa wa mwisho na mkubwa kuliko ya awali. Hakuna mzee aliyekuwa na mchango mpya. Waliposhinikizwa , wote waliinamisha vichwa.Mng'aro wa vipara vyao uliyatia kiwi macho ya kiongozi.Halafu ghafla Mzee Mtepe akapurupuka "Nawauliza ,Wanamatunda ,mzungu wa kula hufundishwa mwana?'Sauti ya Mtepe yenye mkwaruzo ilipasua hewa. "Hapana ",wote wakajibu.Akauliza tena "Dole moja la jitu haliwezi kuvunja chawa?" Baada ya maelezo machache,Mzee Mtepe alihitimisha, "Sisis wenyewe tuna jawabu. Umoja ni nguvu , utengano ni udhaifu .Ama kwa kuti au mauti tuungane tuunde vyama vya ushirika."

Wanamatunda wakaunda vyama vya ushirika .Walivipenda vyama hivi kwa sababu nyingi.Sababu moja ni kuwa walihitajika kutoa pesa kidogo kila siku ,kila wiki au kila mwezi kutegemea utaratibu wa chama.Haba na haba waliweza kujenga hisa.Kila mwisho wa mwaka kila mwanachama alipewa mgao kulingana na kiwango cha faida za chama.

Haya yaliamsha tamaa ya wanachama na muda si muda , vyama vikaanza kustawi huku wanachama wakifurahia huduma mbalimbali. Mojawapo ya huduma ilikuwa mikopo ya dharura kwa wenye shida ya ghafla kama vile msiba au kutindikiwa karo ya shule. Aidha, kulikuwa na mikopo ya maendeleo .Kwayo wanachama walijijengea nyumba au kuanzisha biashara.Wengine walifufua shughuli za kilimo ambazo zilikuwa zimezorota.

Wanamatunda waliweza kupambana na umaskini katika maisha yao.Pesa walizopata zilivunja nguu , milima ikalala.Biwi la mashaka kwa waja hawa liliondolewa nao wakaanza kuishi kama watu.

Wananchi wengi wakapata ari ya kujiandalia maisha bora ya baadaye lakini kumbe ngoma ya wana haikeshi! Viongozi wasio na ujuzi na waliojaa tamaa walivuruga usimamizi wa vyama. Walitumia hila kujipa mikopo mikubwa ambayo hawakuilipa. Halikadhalika waliharibu hazina ya vyama kwa ubadhirifu au matumizi yasiyo mpango. Wengine walipora mali ya wanachama .Kutokana na wizi na wanachama kuchezeshwa ngoma, vyama vilianza kulegealegea na vingine hata kuanguka .Ukweli wa wakubwa kumeza wadogo ulianza kubainika. Wanachama walijuta kwa kutomaizi kuwa paka hawekewi kitoweo kulinda.

Wanamatunda walichelea kurudia ulitima wa hapo awali. Uoga uliwafunza jambo moja muhimu kuwa zindiko la mwoga ni kemi. Wananchi walilia serikali nayo ikaingilia kati. Suala la kwanza halikuwa ngumu.Kwa kuwa ukuni mbaya haufichiki , serikali iliweza kuwatambua viongozi wabaya na kumwondoa kwenye usimamizi wa vyama. Pili, serikali iliagiza vyama vyote visajiliwe rasmi na viunde katiba. Tatu, serikali iliweka vigezo vya

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Teacher.co.ke

watu wanaopaswa kuongoza vyama. Vigezo hivyo vilikuwa elimu, tajriba , maadili na uwajibikaji.

Amri ya serikali , madaftari ya maehasabu ya vyama yalikaguliwa.Pamoja na haya Bunge la nchi ya Matunda lilipisha sharia kali zilizolenga kuwadhibiti viongozi kufuja mali ya vyama.Haya yalikuwa ni pamoja na kuwekwa jela. Mikakati ya vyama kuweka bima ili kukinga hisa za wanachama iliwekwa na punde mapato yao ya mgawo yakaongezeka.

Wahenga walisema kuwa imara ya chombo ni nanga! Uongozi mzuri uliimarisha vyama navyo vikapanuka a kuenea kote nchini. Vingine viliweza kushindana na kanzi za kimataifa. Mara nyingine Wanamatunda wakawa na matumaini ya kuyaboresha maisha yao tena. Kila mmoja alitabasamu alipoukumbuka usemi wa Mzee Mtepe kuwa;'Wawili si mmoja na gezageza ndio mji.'

**Maswali**

a) Kipe kisa hiki anwani mwafaka. (alama 2)

***Vyama vya Wanamatunda***

***Kadiria jibu la mwanafunzi***

b) Kwa nini wazee wote walikuwa vipara ? (alama 1)

***Walipoteza nywele wakijikuna vichwa wakitafuta suluhu ya tatizo lao la umaskini***

c) Ni nini kilichowasukuma Wanamatunda kuunda vyama? (alama 2)

***walikuwa maskini***
***walitakikana kuungana ili kuuondoa umaskini huu***

d) Je, vyama hivi vilikuwa na faida gani kwa jamii hii? (alama 5)

- ✓ ***Havikuwasukuma wanachama kutoa pesa nyingi kwa wakati mmoja***
- ✓ ***Kila mwishoni mwa mwaka wanachama walipata mgao kulingana na faida ya chama***
- ✓ ***Wanachama wangepata mkopo wa dharura***
- ✓ ***Kulikuwa pia na mikopo ya maendeleo***
- ✓ ***Wanachama walijijengea nyumba***
- ✓ ***Walifufua miradi tofautitofauti***
- ✓ ***Walijtoa katika hali ya ulitima***

***Zozote 5*1=5***

e) Eleza mambo matatu yalisababisha vyama vya Matunda kuanguka. (alama 3)

- ✓ ***Viongozi waliokuwa na tamaa na kuchukua mikopo mikubwa ambayo hawakuilipa***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

- ✓ ***Walifuja mali ya vyama***
- ✓ ***Wakawa na matumizi ya pesa bila mpango***
- ✓ ***Wengine waliiba mali ya chama***

***Zozote 3*1=3(kadiria jibu la mwanafunzi)***

f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika taarifa (alama 2)

i) Ngoma ya wana haikeshi-***vyama hivi havingedumu kwa muda***
ii) kwa kuti au mauti-***kwa njia yoyote ile***

**2. UFUPISHO (ALAMA 15)**

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali***

Suala la ukosefu wa kazi miongoni mwa wananchi limekuwa donda sugu linalotishia kukiangamiza kizazi cha leo kwa ulitima usio kifani. Hata hivyo, kila mwananchi ana jukumu la kufanya ili kuhakikisha kuwa nafasi nyingi za kazi zimebuniwa .

Wananchi ambao hawajafanikiwa kupata ajira katika mashirika mbalimbali wanafaa kupewa mkopo na serikali utakaokuwa mtaji wa kuanzisha biashara. Bila shaka wapo wananchi walio na ujuzi wa kuendeleza biashara ila wanachokosa ni mtaji wa kuianzishia biashara yenyewe.Mikopo hii ikitolewa pamoja na riba ya chini, walio na uwezo wa kujiajiri kwa kufanya biashara ndogo ndogo kama vile uchuuzi, ususi na hata useremala wataweza kujivumbulia riziki na kuwaajiri wananchi wengine wasiojua lolote kwenye masuala ya biashara.

Aidha, serikali pamoja na wawekezaji wa humu nchini pasipo na kujenga viwanda vitakavyozalisha mali , tutazidi kununua bidhaa kutoka mataifa yalioendelea.Iwapo serikali na wawekezaji watawekeza kwa viwanda humu nchini basi wananchi watapata ajira aina ainati kama vile za uhandisi , usafirishaji wa mali ghafi yanayotumiwa viwandani, upakiakiaji wa bidhaa na kazi nyinginezo nyingi.Bidhaa kutoka viwanda hivi pia zinaweza kuuzwa katika nchi jirani na serikali kutumia fedha hii kuendeleza sekta kama vile za uchukuzi zit akazowaajiri wananchi zaidi.

Mtalaa wa Elimu wa Nane-nne-nne nao ulichangia kwa kiasi kikubwa ukosefu wa ajira nchini.Mfumo huu haukuangazia kuwapa wanagenzi mbinu za kutumia rasilimali katika mazingira yao ili kujiendeleza na kujitafutia ajira ila kukariri tu nadharia . Mfumo huo pia haukuwazia kuwapa wanagenzi umilisi wa ujasiriamali na stadi za kuwawezesha kujitegemea na kuyadhibiti maisha yao ya baadaye. Hivyo basi hata wale waliohitimu katika viwango vya juu kielmu ,walikimbilia kuandikwa kazi za ofisi ambazo zilikuwa haba na kuselea bila ajira.

Miundo misingi nayo inafaa kuimarishwa nchini. Sekta ya uchukuzi na mawasiliano inafaa kuimarisha kwa kuboresha barabara na hata reli zilizo nchini ili kufikia viwango vya kisasa kwa ubora.Hili itaweza kuhakikisha kuwa wananchi wanaondeleza shughuli za biashara popote pale

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

nchini watasafirisha bidhaa zao kwa urahisi na kuwafikia wateja wao kwa wakati unaofaa na hivyo kuongeza natija yao.

Ni bayana kuwa kwa muda mrefu sasa maendeleo yanayowapa wananchi ajira huwa mijini tu.Maeneo ya mashinani nayo yanafaa kuendelezwa kwa kuanzisha viwanda na hata kujenga barabara bora .Hatua hii itapunguza msukumo wa vijana kukimbilia mijini kwa lengo la kutafuta kazi kwani wataweza kuajiriwa kwa viwanda hivi na hivyo kupunguza tatizo la ukosefu wa kazi mijini. Aidha sehemu zote za nchi zitakuwa sawa kimaendeleo na hivyo basi kutumia rasilimali ya nchi kwa njia endelevu zaidi.

Hata hivyo ,nafasi nyingi za kazi zinaweza kubuniwa kwa kuboresha usalama nchini.Usalama nchini unaweza kuwa njia mojawapo ya kuwavutia watalii na wawekezaji wa kigeni na hivyo basi wenyeji kupata kazi kwenye viwanda vya wawekezaji hawa.Miongoni mwa hatua nyingi ninginezo ,mambo haya yanafaa kutekelezwa kikamilifu na washikadau wote kwenye sekta mbalimbali ili kuliangamiza donda sugu hili la ukosefu wa ajira nchini!

Maswali

a) Kwa maneno kati ya 60-70 fupisha aya tatu za kwanza, (alama 7)

- ✓ ***Kuna tatizo la ukosefu wa kazi***
- ✓ ***Mwananchi ana jukumu la kuhakikisha kuwa nafasi nyingi za kazi zimebuniwa***
- ✓ ***Wananchi ambao hawana ajira wapewe mikopo na serikali kama mtaji***
- ✓ ***Mikopo iwe ya riba ya chini***
- ✓ ***Wananchi kupitia kwa mikopo waweze kufanya biashara***
- ✓ ***Wajivumbulie riziki***
- ✓ ***Waweze kuwaajiri wananchi wengine***
- ✓ ***Serikali iwekeze kwa viwanda vinavyozalisha mali ili kuzua nafasi za kazi zaidi***

***Hoja zozote 6*1=6 na alama moja ya mtiririko***

b) Onyesha sababu zinazochangia ukosefu wa kazi nchini na suluhu za tatizo hili kwa maneno kati ya 90-100. (alama 8)

- ✓ ***Ukosefu wa mtaji-serikali kutoa mikopo ya riba ya chini***
- ✓ ***Uhaba wa viwanda –serikali kuwekeza kwa viwanda vinavyozalisha mali***
- ✓ ***Miundo msingi hafifu-barabara zote na reli kuboreshwa kwa viwango vya kisasa***
- ✓ ***Mtalaa wa elimu usiotegemeka-mtalaa huu uboreshwe na ufunze wagenzi stadi za ujasiriamali na mbinu za kuyaboresha maisha yao***
- ✓ ***Kutelekezwa kimaendeleo katika maeneo ya mashambani-viwanda vijengwe sehemu za mashambani pia***
- ✓ ***Maendeleo yawe kila pahali***
- ✓ ***Usalama nchini-kuwavutia watalii na wawekezaji wa kigeni hivyo kuongeza nafasi za kazi***

***Hoja zozote 7*1=7 na alama moja ya mtiririko***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**

a) Tofautisha kati ya sauti hizi (alama 1)

i) /p/-***sighuna***

ii) /b/-***ghuna***

b) Weka shadda kwa maneno yafuatayo muundo mmoja ili kutofautisha maana za maneno haya (alama 3)

i) Barabara

***ba'arabara-njia ndefu na pana***

***'barabara-sawasawa***

ii) ala

***a'la-kihisishi cha mshangao***

***'ala-aina ya mfuko unaotiwa kisu au upanga***

iii) Walakini

***wa'lakini-kasoro***

***wala'kini- hata hivyo***

Teacher.co.ke

c) Kwa kutolea mfano katika sentensi onyesha dhana zinazobainishwa na kiimbo.(alama 5)

✓ ***Kuuliza swali***

Umetoka wapi?

✓ ***Kutoa kauli***

Chakula kimepikwa.

✓ ***Ombi /rai***

Tafadhali nifungulie mlango.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Teacher.co.ke

- ***Amri/kuamuru***

Ondokeni hapa!

- ***Mshangao***

Ala!Ameyamwaga maziwa yote.

d)Ainisha vitenzi katika sentensi hizi. (alama 2)

i) Kiti ki uwanjani.-***ki-kitenzi kishirikishi kipungufu***

ii) Mwalimu anafunza.-***anafunza-kitenzi halisi***

Teacher.co.ke

d) Ainisha nomino katika sentensi hii. (alama 2)

Kutomakinika kwa Makali kulimfanya aangushe sarafu aliyopewa na mpitanjia.

- ***Kutomakinika-nomino kitenzi-jina***
- ***Makali-nomino ya kipekee***
- ***Sarafu-nomino ya kawaida***
- ***Mpitanjia-nomino ya kawaida***

Teacher.co.ke

f) Ondoa kirejeshi 'amba-' katika sentensi hizi kisha utumie kirejeshi '-o-' kulingana na maelekezo katika mabano. (alama 2)

i) Watu ambao walizawidiwa wamefika.(kirejeshi-o- tamati)

***Watu wazawidiwao wamefika.***

ii) Ukulima ambao unasifika ni huu .(kirejeshi –o- awali)

***Ukulima unaosifika ni huu.***

f) Kwa kutolea mifano tambua miundo mine ya Ngeli ya A-WA (alama 4)

- ***M-WA-Mtoto –Watoto***
- ***MW-W-mwalimu-walimu***
- ***M-MI-Mtume-mitume***
- ***MU-WA-Muuguzi-wauguzi***

***Kadiria jibu la mwanafunzi***

g) Andika sentensi hii kwa wingi (alama 1)

Ufagio uliotumiwa umeharibika .

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

***Fagio zilizotumiwa zimeharibika.***

h) Tambua jukumu la sentensi hii (alama 1)

Nalichukia janadume hili sana.

***Kudharau***

i) Ainisha mofimu katika neno hili (alama 3)

***mlivyowasomesha***

***m-nafsi ya tatu wingi***

***li-wakati uliopita***

***vyo-kirejeshi***

***som-mzizi wa neno***

***esha-kiishio katika kauli ya kutendesha***

k) Bainisha vishazi katika sentensi zifuatazo (alama 4)

i) Kabla ya kung'oa nanga tuliwaombea dua.

***Kabla ya kung'oa nanga-kishazi tegemezi***

***Tuliwaombea dua-kishazi huru***

ii) Licha ya uhaba wa maji ,alioga kila siku.

***Licha ya uhaba wa maji-kishazi tegemezi***

***Alioga kila siku-kishazi huru***

l) Tambua virai katika sentensi hii (alama 4)

Mwajuma wa mwalimu amelazwa hospitali jana jioni.

***Wa mwalimu-RV***

***Mwajuma wa mwalimu-RN***

***Amelazwa hospitali-RT***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

***Jana jioni-RE***

m) Bainisha kiima na kiarifa katika sentensi zifuatazo; (alama 4)

i) Mahindi na maharagwe yanapandwa na mkulima.

***Mahindi na maharagwe-kiima***

***Yanapandwa na mkulima-kiarifa***

ii) Maagizo ya daktari yatawafaa wagonjwa wote.

***Maagizo ya daktari-kiima***

***Yatawafaa wagonjwa wote-kiarifa***

n) Changanua sentensi hii kwa njia ya mshale (alama 4)

Maembe matamu ni ya mkurugenzi.

***S→KN+KT***

***KN→N+V***

***N-Maembe***

***V-matamu***

***KT-t=RH***

***t→ni***

***RH →wa mkurugenzi.***

**4. ISIMUJAMII**

"Mheshimiwa Spika naomba nipewe fursa kutoa maoni yangu kuhusu hoja iliyowasilishwa bungeni na mbunge wa Malishoni Mheshimiwa Patakazi…"

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

i) Weka makala haya muktadha wake. (alama 2)

***Ni mazungumzo yanayofanyiwa katika mazingira ya bungeni*.**

ii) Eleza sifa za mazungumzo yanayofanywa katika muktadha huo uliotaja. (alama 8)

- ✓ ***Kuna kuchanganya ndimi wakati mwingine***
- ✓ ***Matumizi ya lugha ya Kiingereza sanifu hutumiwa hasa katika masuala nyeti kama kusomwa kwa bajeti***
- ✓ ***Matumizi ya uwili lugha hasa katika mijalada bungeni-Kiswahili na Kiingereza***
- ✓ ***Baadhi ya wabunge hawatumii Kiswahili sanifu***
- ✓ ***Urasmi wa matumizi ya lugha hutegemea mada inayozungumzwa***
- ✓ ***Wakati mwingine lugha yenye ucheshi hutumiwa***
- ✓ ***Msamiati wa heshima kama vile Mheshimiwa Mbunge, Mtukufu Rais , Mheshimiwa Spika hutumiwa pale unapokirejelea cheo cha anayehusika***
- ✓ ***Msamiati maalum wa bunge hutumiwa kama vile hoja, spika, maswada, waslisha maoni, mjadala nk***

  ***Hoja zozote 8*1=8***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes